# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Bima,
S.L.P 845,
**67128 MOROGORO**
Simu: 0738 150 143
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe:
rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

---

**MOROGORO MEI, 2022.**

## TAKUKURU MOROGORO YAJIKITA KUDHIBITI FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.

**Ndugu WanaHabari,**

Karibuni katika ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro. Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha tena tukiwa na afya njema. Kama ilivyo ada, nimewaita ili muweze kuujulisha umma, kazi zilizotekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro kwa kipindi cha **miezi mitatu (3)** kuanzia mwezi **Januari 2022** hadi **Machi 2022**.

**Ndugu WanaHabari**

**UCHUNGUZI NA MASHTAKA**

Katika kipindi cha Mwezi **Januari 2022** hadi **Machi 2022**, tulipokea jumla ya taarifa **101** na kati ya hizo, taarifa **52** zilihusu vitendo vya rushwa na kufunguliwa majalada ya uchunguzi. Uchunguzi wa majalada haya bado unaendelea. Taarifa **49** ambazo hazikuhusu rushwa, watoa taarifa hao walishauriwa jinsi ya kufuatilia malalamiko yao pamoja na kuwatatulia kero zao kwa kuwapeleka kwenye mamlaka husika.

Taarifa 101 zilizowasilishwa, zilihusu maeneo yafuatayo:

**Sekta 18** zililalamikiwa huku sekta iliyoongoza katika kulalamikiwa ikiwa ni Tamisemi- Utawala ikifuatiwa na sekta nyingine kama zilivyoainishwa hapa chini:- TAMISEMI – UTAWALA **(19),** ARDHI **(14),** WATENDAJI WA VIJIJI, MITAA NA KATA **(12),** POLISI **(08),** MAHAKAMA **(08),** UJENZI (06), SEKTA BINAFSI **(06),** TAASISI ZA FEDHA **(05),** KILIMO **(05),** ELIMU **(04),** MAJI **(04),** AFYA **(04),** MABARAZA YA KATA **(03),** MADINI **(02)** na AMCOS **(01).**

Katika kipindi tajwa, kesi mpya **Nne (04)** zimefunguliwa Mahakamani na kufanya jumla ya **kesi 27** zinazoendelea Mahakamani. Aidha kesi **tatu (03)** ziliamuliwa ambapo Jamhuri ilishinda kesi **Mbili (02)** na kesi **Moja (01)** iliondolewa kwa mujibu wa taratibu za kimahakama.

**Ndugu WanaHabari,**
**ELIMU KWA UMMA**

Katika kipindi cha kuanzia mwezi **Januari 2022** hadi **Machi 2022**, kupitia Dawati la Elimu kwa Umma, tumefanya kazi zifuatazo:- Mikutano ya Hadhara na Mijadala ya Wazi **Arobaini na Nne (44), semina** kwa wananchi na watumishi wa umma **Kumi na Mbili (12),** uimarishaji wa Klabu za wapinga rushwa wa shule za msingi, sekondari na vyuo **Tisini (90),** Vipindi vya Redio na TV **Vitano (05),** Maonesho **Matano (05),** Uandishi wa Makala **kumi na Tatu (13)** Utoaji wa habari kwa umma kupitia vyombo vya habari Moja **(01).**

**Ndugu WanaHabari**
**TAKUKURU INAYOTEMBEA**

Katika kipindi tajwa hapo juu TAKUKURU ilitembelea Shule ya Msingi Kigurunyembe kwa ajili ya kuongea na wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo kufuatia malalamiko ya uwepo wa michango ya mlinzi, maji na umeme. Katika kikao hicho wazazi walitoa ufafanuzi kwamba wao kama kuna michango itasimamiwa na wazazi wenyewe na hawatahusisha walimu wa shule hiyo.

**Ndugu WanaHabari**
**Utekelezaji wa Mpango Kazi wa TAKUSKA.**
Katika kipindi tajwa hapo juu, TAKUKURU ilikamilisha kazi ya kukabidhi vitabu vya Mwongozo wa Mafunzo kwa Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro na kutoa semina kwa vijana wa Skauti.

**Ndugu WanaHabari**
**Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**
Katika kipindi cha Mwezi **Januari 2022** hadi **Machi 2022,** tulifanikiwa kufuatilia jumla ya Miradi ya Maendeleo 20 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 27.347.** Miradi hiyo iko katika sekta za **Ujenzi, Maji, Afya, Elimu na Mifugo.**

Katika ufuatiliaji huo, TAKUKURU imeweza kudhibiti jumla ya **shilingi** milioni **6.46** zilizofanyiwa ubadhirifu na watumishi wachache wasiokuwa waaminifu katika usimamizi wa ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa, ofisi na matundu nane (8) ya choo yaliyokuwa na thamani ya Shs. Milioni 48.8. Katika kupitia nyaraka za malipo ilibainika kwamba, kiasi halisi kilichokuwa kimelipwa kilikuwa ni kidogo kuliko malipo yaliyofanyika. Aidha licha ya nyaraka kuonyesha kuwa malipo yalikuwa yamefanyika kwa mafundi lakini mafundi walidai kutolipwa fedha zao.

**Ndugu WanaHabari**
**Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko 19.**
Katika kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imefuatilia jumla ya **miradi 11** yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 2. 255** katika sekta za **Afya** na **Elimu.**

Katika ufuatiliaji huo, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro ilibaini kuwa mradi mmoja wenye thamani **ya shilingi 250,000,000.00** unaohusu ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi katika Hospitali ya Wilaya ya Kilosa, lilionekana kuwa na kasoro ya matumizi ya tofali zisizofaa. Wahusika walishauriwa kutumia tofali zenye kiwango na ushauri huo ulizingatiwa na kazi inaendelea.

**Ndugu WanaHabari**

**Uchambuzi wa Mifumo**

Katika kipindi cha **Januari 2022** hadi **Machi 2022** TAKUKURU Mkoa wa Morogoro tumefanya chambuzi za mifumo **Kumi (10)** za viashiria vya rushwa katika sekta za Elimu (rushwa ya ngono, uhamisho wa watumishi, usimamizi wa mtihani), ujenzi – TEMESA (matengenezo ya magari), Fedha (Ukusanyaji wa mapato, ushuru wa madini ujenzi,). Vikao vya wadau (warsha 5) vilivyojadili na kuweka maazimio ya namna bora ya kuondokana na mianya hiyo ya rushwa vimefanyika.

**Ndugu WanaHabari**

**Maadhimisho ya Wiki ya Sheria mwaka 2022**

TAKUKURU Mkoa wa Morogoro ilishirikiana na wadau wengine katika maadhimisho ya wiki ya Sheria yaliyofanyika kuanzia tarehe 24/01/2022 hadi 02/02/2022 katika Manispaa ya Morogoro. Maadhimisho hayo yalikuwa na kauli mbiu isemayo **"Zama *za mapinduzi ya nne ya viwanda: safari ya maboresho kuelekea Mahakama Mtandao*"**.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, TAKUKURU ilitumia wiki hiyo kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa katika shule za msingi na sekondari, vyombo vya habari (Radio na TV), kutembelea magereza pamoja na onesho lililofanyika katika viwanja vya Faya. Wananchi waliohudhuria katika banda la TAKUKURU walielimishwa kuhusu umuhimu wa ushiriki wao katika kuvitokomeza vitendo vya rushwa ikiendana na Kauli Mbiu ya TAKUKURU inayowataka wananchi wote waone kuwa ni Jukumu la kila mmoja katika Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

**Ndugu WanaHabari**

**Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2022**

Kila mwaka ifikapo tarehe 08 Mwezi Machi Tanzania huungana na Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuadhimisha siku ya wanawake Duniani. Mwaka 2022 maadhimisho hayo yalikuwa na kauli mbiu isemayo ***"…Kizazi cha usawa kwa maendeleo endelevu…"*** ambapo TAKUKURU ilitumia

siku hiyo kuwakumbusha wanawake juu ya wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa kwa na kuwasisitiza wawe mstari wa mbele katika kupiga vita rushwa kwa lengo la kujiletea maendeleo.

**Ndugu WanaHabari**

**Mikakati kwa kipindi cha Aprili 2022 – Juni 2022** ni kama ifuatavyo:-

**Kwanza**, tunaendelea kufuatilia fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili ziweze kutumika kutokana na malengo yaliyokusudiwa. Niwakumbushe wasimamizi wote wa miradi ya maendeleo kuwa waaminifu na wadilifu katika kusimamia miradi hiyo ili iweze kuleta tija kwa Taifa. TAKUKURU Mkoa wa Morogoro haitasita kuchukua hatua dhidi ya wote watakaofuja fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Pili,** kuchunguza taarifa za ubadhirifu wa fedha zilizotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika baadhi ya Taasisi za Serikali, ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

**Tatu,** tunaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa jamii kupitia mpango wa **TAKUKURU INAYOTEMBEA** kwa kufanya mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi, semina na vyombo vya habari. Tunaamini elimu hii ikitolewa kwa kiwango kikubwa itasaidia kudhibiti vitendo vya rushwa vinavyojitokeza katika utekelezaji wa majukumu. Nitoe rai kwa wananchi kuhudhuria kwa wingi katika mikutano na mijadala ya wazi inayosimamiwa na TAKUKURU kwa ajili ya kusikiliza na kutoa kero zao kupitia mikusanyiko hiyo kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Aidha TAKUKURU pia itaendelea kushirikiana na SKAUTI katika kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na uzalendo kwa vijana walioyoko mashuleni na wale ambao hawako katika mfumo rasmi wa elimu.

**Ndugu WanaHabari**

Ifahamike kuwa jukumu la kuzuia na kupambana na Rushwa ni la kila mmoja wetu, hivyo hatuna budi wote kwa pamoja pasipo kujali itikadi za vyama, dini, mila, rangi wala ukabila kushirikiana katika udhibiti wa vitendo vya rushwa. Tunaamini kuwa kwa umoja huo tunaweza kuitokomeza rushwa nchini.

**Ndugu WanaHabari,**
Nitumie fursa hii kuwakumbusha watumishi wa umma na sekta binafsi katika Mkoa wetu wa Morogoro, kuwa waadilifu na waaminifu wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao kila siku, wajiepushe na matumizi mabaya ya madaraka, ubadhirifu wa fedha za umma na kudai rushwa kutoka kwa wananchi kama sharti la kuwahudumia.

Aidha ninatoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro na Wilaya zake kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa zote za vitendo vya rushwa pamoja kufuatilia kwa karibu miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao na kuitolewa taarifa katika Ofisi ya za TAKUKURU kwa kufika katika ofisi zetu ambazo ziko kila wilaya au kwa kupiga simu ya bure **113**, ujumbe mfupi wa maandishi ***113#** au kupiga simu kwa Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro namba **0738150143.**

Aidha wananchi waliopo Wilayani wanaweza kuwasiliana na Wakuu wa TAKUKURU Wilaya kwa namba zifuatazo:- Kilombero **0738 150 145,** Kilosa **0738 150 146;** Mvomero **0738 150 147**, Ulanga **0738 150 148;** Malinyi **0738150149** na Gairo **0767 531 177.**

***....Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza...***

**Imetolewa na:-**

Manyama Tungaraza
**Mkuu wa TAKUKURU Mkoa**
**MOROGORO**
**SIMU: 0738150143**